COUNTY MOCK EXAMS-STD 8
2016

KISWAHILI PAPER

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

BARINGO COUNTY
KOIBATEK MTIHANI WA MWIGO
DARASA LA NANE - 2016
SEHEMU YA KWANZA:KISWAHILI

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO **Muda: Saa 1 dakika 40**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina Maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu.

NAMBA YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika kisanduku zenye namba zinazokuhusu. Onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa Herufi A. B. C. D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Kwa mfano:

Katika kijitabu cha maswali

30. Mori ni kwa fahali ilihali koo ni kwa
    A. tembe
    B. pora
    C. jimbi
    D. mbarika

Jibu sahihi ni C

Katika karatasi ya majibu:

29 (A) (B) (C) (D) 30. (A) (B) ~~(C)~~ (D) 31. (A) (B) (C) (D) 32. (A) (B) (C) (D)

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 30, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne uliyopewa.

FUNGUA UKURASA

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15 kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi ya yale uliyopewa

Vijana wanapaswa wielewe ___1___ wa kurekebishwa tabia. Hakuna haja ya kijana kufura kama hamira ___2___. Mtu akikukanya jambo usichukulie kuwa hakupendi na ___3___ usimfanyie kiburi kwani kufanya hivyo ni kinyume cha uungwana,na ukamkatisha tamaa mwenye ___4___. Ifahamike kuwa muungwa hanuni mashavu hununa ___5___. Ni lazima vijana watamoue kuwa hata wazazi wao walirekebishwa tabia ___6-___ zamani. Walipewa ___7___ kali hata kuliko zile wanazopewa leo. Jambo la kushangaza ni kwamba hawakuwanunia wazazi wao bali waliwapa mkono wa ___8___

1.	A. ufahamu	B. maelngo	C. umuhimu	D. wajibu
2.	A. anapoaswa	B. anapoasisis	C. anapoasa	D. anapoasiwa
3.	A. bali	B. ingawa	C. hata	D. wala
4.	A. kukurudufu	B. kukurufai	C. kukurudi	D. kukurudia
5.	A. usoni	B. tumboni	C. moyoni	D. machoni
6.	A. yao	B. zao	C. wao	D. lao
7.	A. adabu	B. mashauri	C. adhabu	D. somo
8.	A. heri	B. kongole	C. buriani	D. tahania

Baraza la taifa ___9___ mtihani sasa limebuni mpango ___10___ watahiniwa waliokosa mitihani au matokeo yao watafanya mtihani ___11___ matokeo ___121___. Kulingana na Afisa Mkuu Mtendaji, watahiniwa hap wataruhusiwa kufanya mitihani yao ya darasa la nane na ___13___ cha nne, kati ya Februari na Machi. hatua hiyo imechukuliwa ikizingatiwa kuwa watahiniwa ___14___ kusubiri mwaka ___15___ kabla kufanya tena mtihani.

9.	A. la	B. ya	C. wa	D. kwa
10.	A. ambayo	B. ambao	C. ambapo	D. ambavyo
11.	A. punde	B. kama	C. punje	D. ikiwa
12.	A. yanatangazwa	B. yatakapotangazwa	C. yalipotangazwa	D. yanapotangazwa
13.	A. kidaka	B. kidatu	C. kidete	D. kidato
14.	A. hulazimika	B. hulazimu	C. hulazimisha	D. hulazimia
15.	A. nzima	B. mzima	C. zima	D. mizima

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi

16. **Wingi wa sentensi:**
Mkoba wake ulichukuliwa na mpagazi.
A. Mikoba zao zilichukuliwa na mapagazi
B. Mikoba yenu ilichukuliwa na wapagazi
C. Mikoba yao ilichukuliwa na wapagazi
D. Mikoba zenu zilichukuliwa na wapagazi

17. Chagua mpangilio sahihi wa viakifishi vifuatavyo:
(:) (*) (.) (...)
A. nukta mkato, dukuduku, kipumuo, ritifaa
B. nukta pacha, ritifaa, koma, dukuduku
C. nukta koma, king'ong'o, kipumuo, ritifaa
D. nukt mkato, ritifaa, koma, dukuduku

18. Nazi iliyokunwa huitwa:-
A. ufu B. machicha C. tui D. kifuu

19. Udogo wa: Mbwa alimuuma mvulana ni:
A. Kijibwa kilikiuma kivulana.
B. Kijijibwa kilikiuma kijivulana.
C. Kijibwa kilikiuma kijivulana
D. Kijijibwa kilikiuma kivulana.

20. Chagua sentensi yenye matumizi sahihi ya 'na' ya uhusiano.
A. Hapa napo ni safi B. Wajenzi wana ujuzi
C. Tuna walimu wazuri D. Wanasoma kwa bidii

21. Chagua jibu lenye maelezo sahihi:
A. Mcheja - jina wanaloitana wazazi wa mume na mke
B. Mavyaa - mama wa mume
C. Kivyere - baba au mama wa mke au mume
D. Mwamu - mtoto wa amu

22. Chagua usemi taarifa wa
"Mtu huyu ni mrefu ajabu," mtoto alisema.
A. Mtoto alijabia urefu wa mtu huyo.
B. Mtu huyo alikuwa mrefu ajabu mtoto alisema
C. Mtoto alisema kuwa mtu huyo alikuwa mrefu ajabu
D. Mtu huyu ni mrefu ajabu mtoto alisema

23. Chagua neno lililoambatanishwa na nomino husika kwa usahihi
A. Nomono za wingi - manukato
B. Nomino dhahania - halaiki
C. Nomino za pekee - kuika
D. Nomino za kawaida - masakhwe

24. Neno lipi lenye sauti mwambatano.
A. Cheka B. Ruka C. Mtuko D. Ziba

25. Neno 'msalani' lina silabi ngapi?
A. 3 B. 4 C. 5 D. 8

26. Kukanusha kwa:
'Wanafunzi waliofuzu walituzwa' ni:
A. Wanafunzi wasiofuzu walituzwa.
B. Wanafunzi waliofuzu hawajatuzwa.
C. Wanafunzi wasiofuzu hawakutuzwa.
D. Wanafunzi waliofuzu hawakutuzwa.

27. Ni jibu lipi lenye vivumishi halisi pekee?
A. lenye, wote, wengi, yyote
B. bichi, gumu, safi, yetu
C. wangu, wetu, changu, vyenu
D. chote, jingine, mwenyewe, lolote

28. Chagua malipo yasiyoambatanishwa na maelezo yake kwa usahihi.
A. Karadha - mkopo usiotozwa riba
B. Mrabaha - malipo anayopewa mwandishi.
C. Dia - malipo ya kutolewa damu.
D. Mapoza - malipo kwa ajili ya hasara.

29. Ni nini maana ya walibishana?
A. Mimbishia naye akabisha
B. Walishirikiana kubisha
C. Walipingana kwa maneno
D. Waligongeana mikango

30. Watu hao wamefanana kama:
A. shilingi kwa shilingi B. pacha
C. shilingi kwa ya pili D. tui na maziwa

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 31-40

Wanasayansi wengi wameshindwa kuelewa ni kwa nini watu huvuta sigara. Jambo hili limewatatiza binadamu kwa kame nyingi zilizopita na kuwatachia rundo la maswali hukusu uvutaji sigara.

Sigara au sigareti ni kitu cha uraibu wa kuvuta, kinachotengenezwa kwa majani ya tumbaku yaliyokaushwa. Husokotwa katika karatasi maalumu. Majani ya tumbaku pia huvutwa kwenye kiko, hunuswa na kutafunwa. Tumbaku inayosagwa na kunuswa huitwa ugoro.

Hapana shaka wavutaji sigara huharibu afya yao Wataalamu wa sayansi na madaktari wamefanya uchunguzi na wamethibitisha kuwa moshi wa sigara huathiri wavutaji wa sigara na watu walio karibu nao na pengine huleta ugonjwa wa moyo. Wavutaji hupatwa na kikohozi cha daima kisichosikia dawa; mwishowe hupata maradhi mfano wa pumu kutokana na moshi wa sigara unaowakereketa koo. Kuna pia wanaosema kwamba uvutaji wa sigara unasababisha saratani ya mapafu. Watu wengi hufa kwa ugonjwa wa ghafla kwa sababu ya sumu ya moshi wa sigara ambao huyaunguza na kuyatoboatoboa mapafu.

Baadhi ya wavuta sigara waweza kuonekana wameungua midomo kwa sababu ya kuvuta vipande vya sigara. Vipande hivyo, vinavyotupwa ovyo bila kuzimwa husababisha hasara kubwa kama vile uchomaji wa msitu, nyumba na nguo na wakati mwingine husababisha hata vifo. Uvutaji sigara umefika kiwango cha kusikitisha. Utaona vijana, yaani wasichana na wavulana wadogo sana wakivuta sigara mbele ya watu wazima bila kujali. Hii ni aibu kubwa sana.

Tabia hii inatokana na mifano wanayoiona kutoka kwa wazazi au watu wengine. Si ajabu kumsikia mzazi akimtuma mwanawe akamnunulie pakiti ya sigara au kopo la tumbaku. Wazazi kama hao huwafanya watoto wao wavute sigara ili nao wajione kama watu wazima.

Sababu nyingine ya kuvuta sigara ni fahari tu ya kutaka kujionyesha ati wana nakidi na kwao, huo ni umaarufu. Hivyo basi, sigara hazifai kupatiwa matangazo yenye kuvutia kwa vijana.

Aina nyingine ya uraibu ni uvutaji wa bangi. Bangi ni aina ya majani ya mmea fulani yanayolevya na kupumbaza akili yanapotafunwa au kuvutwa. Wavuta bangi kwa hakika hupatwa na balaa kubwa mwilini, kukonda na huvuruga akili wasijue wanalolifanya. Wataalamu husema bangi ikiingia akilini huharibu kitivo cha fikira mpaka mtu huwa kama mwendawazimu.

Ni muhimu wazazi na walimu wawakataze na wawakanye watoto wasishiriki tabia hizi mbaya.

31. Kulingana na aya ya kwanza:
A. wanasayansi wamepata suluhisho la watu kuvuta sigara
B. watu wametingwa na sababu nyingi wanapovuta sigara
C. tatizo la uvutaji wa sigara limeshindwa kutatuliwa
D. wanasayansi hawajapata kufahamu kichachosababisha watu kuvuta sigara

32. Chagua jibu lisilo sahihi kulingana na kifungu:
A. majani ya tumbaku hutumiwa kutengeneza sigareti
B. sigara hu[illegible] na mazoea mayo
C. Hutia sumu mwilini, kumpa mtu starehe na kupata pumu
D. Husababisha vifo na kufurahisha mvutaji moshi unapopaa

34. Kifungu kimebainisha kwamba watu wengi;
A. wanajaribu kuiga wenzao wanaposutwa kuvuta sigara
B. hufariki ghafla kwa kuathiriwa na sumu ya moshi wa sigara
C. wanakereketwa koo na kupata nafuu baada ya kuacha sigara.
D. wamefanyiwa uchunguzi wa mapafu

35. Ni jibu lipi sahihi kulingana na aya ya nne?
A. Si wote walioungua midomo ni wavuta sigara
B. Sigara husababisha uzorotaji wa tabia
C. Uvutaji sigara hausikitishi vile
D. Vijana wakubwa ndio huvuta sigara mbele ya watu wazimu

36. Kulingana na aya ya tano:-
A. wazazi wamechangia pakubwa kwa wana wao kuvuta sigara
B. utazamaji wa runinga umeathiri wavuta sigara
C. watu wazima huwapa watoto sigara
D. watoto hupewa fursa ya kuwaiga watu wazima

37. Sigara hazifai kupatiwa matangazo yenye kuvutia kwa vijana kwa sababu:-
A. wengi wao hujionyesha mno jinsi wanavyojua kuivuta
B. wengi hupata pesa nyingi
C. hufanya wachuuzi kupata pesa zisizo halali
D. huwafanya walichukulie jambo hilo kuwa la kifahari na la kimaarufu.

38. Wataalamu wamebainisha kwamba uvutaji wa bangi;
A. hupumbaza akili
B. hulevya mtumiaji
C. humkondesha mvutaji
D. huweza kumtia mtu wazimu

39. Mtazamo wa mwandishi katika aya ya mwisho ni kwamba:
A. sigara ni nzuri kwa watoto wachanga
B. wanasayansi hawajapata namna ya kuwazuia wavuta sigara
C. walimu na watu wazima watafute mbinu za kuzuia uvutaji sigara
D. wazazi na walimu washirikiane katika kuwaonya watoto dhidi ya mienendo mibaya maana ya 'balaa'

40. Kulingana na kifungu ni:
A. huleta manufaa mwilini B. huvutia sifa mwilini
C. huchangia ukuaji wa mwili D. kupunguza mwili

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.

Hapo zamani katika shule ya Rebuoni alikuwepo mwanafunzi aliyeitwa Hemedi. Hemedi alikuwa kijana wa kiume mwerevu mno. Daima, alishikilia nafasi ya kwanza katika darasa lake. Miguu ya Hemedi ililemaa na ilimbidi kuchechemea alipotembea kasoro hii iliwafanya wanafunzi wengine kumbagua kwani asingeweza kucheza michezo waliyocheza wenzake kama kandanda kutokana na ulemavu huo.

Akiwa shuleni, nyakati nyingi Hemedi alipandwa na jazba alipofanyiwa masihara na wenzake lakini dua la kuku halimpati mwewe. hasira za hemedi ziliambulia patupu. Alipiga moyo konde na kutulia tuli kama maji ya mtungi ingawa kila wakati alirushiwa kejeli zilizomkera mno.

Mwalimu mkuu wa shule aliwaonya wanafunzi watukutu dhidi ya kumdunisha na kumdhihaki Hemedi. Nyakati nyingi aliwacharaza mijeledi waliomfanyia mzaha hemedi lakini kunao ambao walikuwa kama vyombo vya kuzama ambavyo havina usukani. bongo tupu alikuwa mmoja wao.

Hemedi alijitahidi katika masomo yake na mwishowe akafaulu katika mtihani wa mwisho na kujipatia nafasi katika shule ya upili ya Pambazuko. Shule hii ilitia fora kwa matokeo mazuri katika mitihani ya kitaifa.

Ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni. Maisha ya Hemedi katika shule ya upili yalikuwa biwi la simanzi tupu. Wanafunzi wa madarasa ya juu waliminyanya sa kwa kumbandika majina ya kebehi kama vile 'kiguru', 'miguu beni' na mengine yaliyomkera maskini. Mara si haba machozi yalimdondoka machoni, ghadhabu ikamsakama moyoni na maisha yakawa kama wingu la kiza kingi. Miongoni mwa waliomwandama Hemedi kwa matusi. Bongotupu ndiye aliyekithiri. Alikuwa amepata nafasi ya kidato cha kwanza katika shule ya Pambazuka kwa njia haramu kwani wazazi wake walikuwa wakwasi na hapo wakaweza kuzunguka mbuyu ingawaje hakuwa amehitimu alivyopasa katika mtihani wake.

Bongotupu alikuwa kijana wa kimo cha wastani, mwenye haiba ya sura iliyopendeza na kiburi kilichompofusha. Katika masomo, Bongotupu alikuwa haambiwi chochote. Darasani alisinzia oyyo. Alikuwa bozi kama konokono. domo kaya aliyemzidi chiriku na mropokaji asiyechoka.

Bongotupu hakumpa utulivu wowote Hemedi. Alimtusi bila sababu. Hemedi aliupiga moyo konde, kweli mkono usioweza kuukata ubusu. Bongotupu hakukoma, alichacha kila kulipokucha. Alimwaibisha Hemedi kila alipopata nafasi na hasa mbele ya wasichana kwani shule yao ilikuwa ya mseto. Wasichana wengi waliokuwa mashabiki wa Bongotupu walimcheka mno Hemedi alipotukanwa. Mmoja wa hawa aliitwa Halima. mpenziwe Bongotupu.

Hali hii iliendelea hadi wakati wa kufanya mtihani wa mwisho wa shule ya upili ulipowadia. Mtihani ulifanywa na baada ya miezi miwili, matokeo yalitangazwa. Hemedi alikuwa amefaulu vizuri sana. Bongotupu na Halima walikuwa wameanguka miguu juu.

Hemedi aliendelea na masomo katika chuo kikuu. Alisomea kitivo cha sheria. Mwishowe alihitimu vizuri akawa hakimu. Alifanya kazi kwa bidii. Naye Mungu hamwachi mja wake. Alianza kupata ukwasi. Baada ya miaka michache, alinunua gari na kumwajiri dereva. Sasa aliheshimika karibu na mbali.

Kweli bahari haishi zinge! Siku moja Hemedi alikuwa mahakamani. Mbele yake palifikishwa mtu aliyeshtakiwa kwa kuiba kwa kutumia mabavu. hemedi alimwangalia mshukiwa kwa makini. Mtu huyu alikuwa na uso wa makunyanzi kama wa mzee wa miaka mia moja, na tena mwenye hasira! Hemedi alivua miwani yake na kumwangalia mtu yule kwa makini zaidi. Lo! Bongotupu.

Hemedi alimsaili mshukiwa na mwishowe kumpata na hatia. Mshtakiwa alihukumiwa kifungo cha mwaka mmoja na kuchapwa vikobo saba. Kila mshtakiwa kuelekezwa jela. Hemedi alimwita na kumwuliza, "Je wewe unanikumbuka?" Mshtakiwa alyaanguza macho yake na kupigwa na kibaharati. Kama mwenye kigugumizi, mshtakiwa alitamka,

"wewe si ni wewe ni He Hem tulikuwa nawe.....si wewe ni..... Hemedi! Naye hemedi alimwangalia kwa macho yaliyojaa huruma na kumwambia, "kumbuka yote uliyonifanyia tulipokuwa shuleni pamoja, daima usimcheke kilema.

41. Ni jambo lipi lililowafanya wanafunzi wengine kujitenga na Hemedi?
    A. Kushikilia kwake nafasi ya kwanza darasani
    B. Kuwaripoti wenzake kwa mwalimu mkuu
    C. Kucheehemea kwake alipotembea
    D. Kuwa mwenye hasira
42. Kupandwa ladhba kwa Hemedi kulitokana na nini?
    A. Kubuguliwa na wenzake katika michezo
    B. Kufanyiwa masihara na wenzake
    C. Mwalimu mkuu kuwarudi wenzake
    D. Kunawiri katika masomo yake
43. Maneno kuzunguka mbuyu yanamaanisha:-
    A. kuzunguka mti B. kuomba msaada
    C. kutembelea mganga D. kutoka hongo
44. Mwalimu mkuu wa shule ya Rebuoni hakufanya nini kumsaidia Hemedi?
    A. Hakuwaonya wanafunzi watukutu
    B. Hakuwacharaza waliomfanyia mzaha Hemedi
    C. Hakuwapa ushauri nasaha wanafunzi wasumbufu
    D. Hakumwadhibu wanafunzi watukutu
45. Ni nini maana ya usemi 'domo kayo'?
    A. Mwenye kuleta vurugu
    B. Mwenye kubeba mambo kifuani
    C. Mwenye kusaili mambo
    D. mwenye maneno mengi
46. Ni jibu lipi sahihi kulingana na taarifa?
    A. Kasoro ya maumbile si changamoto ya kufuzuia kufanikiwa maishani.
    B. Tuwaheshimu wenye ukamilifu pekee
    C. Tusicheze na wenye ulemavu huenda tukawajeruhi
    D. Tuwabeze wenye kasoro ili wawe na adabu
47. Kulingana na kifungu ni ipi si sifa ya shule ya pambazuko?
    A. Huwasajili wanafunzi wenye jinsia zote
    B. Ilifanya vyema katika mitihani ya kitaifa
    C. Wanafunzi wawaheshimu na kuwajali wenzao
    D. Wanafunzi waliwabandika wenzao majina ya kebehi
48. Kauli 'bahari haishi zinge' ina maana gani?
    A. Mabadiliko hayana mwisho
    B. Kukutana na mwingine mahakamani
    C. Kuiba kwa kutumia mabavu
    D. Kuwa na uso wa makunyanzi
49. 'Kumbuka yote uliyonifanyia tulipokuwa shuleni pamoja....." Maneno haya yanarejelea usemi:
    A. anayeonja asali huchonga mzinga
    B. anayepanda kilele, hupiga kelele
    C. ashibaye hamjui mwenye njaa
    D. anayenyolewa kwa chupa hasahau
50. Kichwa kinachofaa zaidi kifungu hiki ni:-
    A. Changamoto za shule za mseto
    B. Madhara ya kutoa hongo
    C. Mchela kilema hafi hakijamfika
    D. Vituko mahakamani